# OFISI YA RAIS - TAMISEMI
## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

OFISI YA MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI ZOMBO,
S.L.P 169,
Simu: 0786 483150,
**KILOSA.**

Tarehe ......... /....... /2020.

Kumb. Na. KDC/ZSS/REG/020/ .........

Jina la Mwanafunzi ....................................................
.........................................................................................
S.L.P ..................................

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ZOMBO WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021.</u>**

**1.0 UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha KWANZA katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari ZOMBO ni shule ya **KUTWA,** ipo umbali wa km 18 Kusini Magharibi mwa Mji wa Halmashauri ya Wilaya ya KILOSA Usafiri wa basi kutoka Mjini unapatikana kituo cha mabasi Kilosa mjini kwa nauli ya Tsh.3000/-

Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe 11/ 01 / 2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11 / 01 / 2021; Mwisho wa kuripoti ni tarehe 22 / 01 / 2021 ndani ya siku 14.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

2.1 **Sare za Shule;**

(a) Wavulana ni **SURUALI YA KIJANI 2** (zenye malinda mawili na pindo chini(16)na zisizobana chini), **SHATI NYEUPE MBILI 2, VIATU VYEUSI VYA KAMBA 2** (kisigino kifupi), **SOKSI NYEUPE.**

(b) Wasichana ni **SKETI ZA KIJANI 2** ( zinazovuka magoti zenye malinda matatu), **SHATI NYEUPE 2, VIATU VYEUSI VYA KAMBA 2** (kisigino kifupi ), **SOKSI NYEUPE.** (Kipande cha kitambaa kimeambatanishwa) .

(c) Wasichana wa Kiislam wanashauriwa kuvaa **Hijab**; suruali zishonwe kwa kuzingatia Sare za Shule.

**NB:** Nusu kanzu ndefu nyeupe (tetroni) mikono mirefu isiwe na urembo wowote.
Kijuba / mtandio mweupe (tetroni) usiokuwa na urembo wowote.

(d) Fulana yenye Nembo ya shule rangi Damu ya Mzee, Tai na Sweta la Kijani.

(e) Sare ya Michezo kwa wavulana rangi Bluu bahari, na kwa wasichana rangi Nyekundu (trakasuti / kaptula na tisheti).

(f) Viatu vya michezo raba rangi nyeupe / nyeusi.

2.2 **Mahitaji mengine:**

1. Counter Book Q3 (9), Kalamu, Rula na mkebe wa hesabu.
2. Nauli / usafiri wa mwanafunzi kuja shuleni na kurudi nyumbani ni jukumu la mzazi.
3. Mahitaji mengineyo ya kibinadamu ( kama yapo mpe mwanafunzi).

Scanned with CamScanner

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye Dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu Nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi / walimu wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni( preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Na
(i) Kutunza mali za umma / shule.

### 3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha Mwanafunzi kufukuzwa au kusimamishwa shule.

(a) Wizi.
(b) Uasherati na ushoga.
(c) Ubakaji.
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupiga au kupigana.
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma / shule.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
(i) Kuoa au Kuolewa.
(j) Kutoa mimba.
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na simu ya mkononi

### 3.2 Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi;

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Form ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi na Mkataba wa Kutoshiriki katika Migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Form ya **Mzazi Kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule**.

4.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

.............................................

Mwl MBOJE LEONIS BANGILI
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
ZOMBO SECONDARY SCHOOL

THE HEADMASTER
ZOMBO SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 169 KILOSA

Scanned with CamScanner

# PRESIDENT'S OFFICE
# REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
# KILOSA DISTRICT COUNCIL
# ZOMBO SECONDARY SCHOOL

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**FROM:** The Medical Officer
Government Hospital ...................................
.............................................
.............................................
.............................................

**To:** The Headmaster,
ZOMBO Secondary School,
P.O.Box 169,
**KILOSA.**

**RE: MEDICAL CERTIFICATE**
**(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined ................................................... Who aspires to join form one (I) in your school as follows:

| | AREA | REMARKS |
|---|---|---|
| 1. | Skin | ............................................ |
| 2. | Eyes | ............................................ |
| 3. | Ears | ............................................ |
| 4. | Teeth | ............................................ |
| 5. | Chest | ............................................ |
| 6. | Spleen | ............................................ |
| 7. | Abdomen | ............................................ |
| 8. | Urine | ............................................ |
| 9. | Tool | ............................................ |
| 10. | HB Haemoglobin | ............................................ |
| 11. | Sickle cell | ............................................ |
| 12. | Asthma | ............................................ |
| 13. | Pregnancy for Girls | ............................................ |
| 14. | Any other comments | ............................................ |

..................................................................................

I consider that he/she is physically / not physically fit to join your school due to ..............................
.....................................................................................................................

Signature: ............................................ Date: ...................... Official Stamp: ............................

Scanned with CamScanner